# UQAB

Jarida la



*Toleo 19 - Dhul Qaadah 1439 AH / Agosti 2018 Miladi*

**Suluhisho la Matatizo yanayoikumba Sekta ya Elimu**

**Nigeria Yakabiliana na Mustakbali Usiothabiti**

**Sakata ya Sukari**

**Marekani Inapaswa Kujifunza Kutokana na Uhuru wake**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 15**

**SWALI/JAWABU: Kongamano la Maraisi Baina ya Amerika na Korea Kaskazini**



## Hatari ya Uvivu na Ukosefu wa Motisha kwa Muislamu

uqab.or.ke   uqab_htk   uqab_htk   UQAB-Magazine-1911964012162253

# Hatari ya Uvivu na Ukosefu wa Motisha kwa Muislamu



Kila mmoja anaijua hali ambayo mtu anajihisi ulegevu fulani na kutokana na hisia hii inakuwa vigumu kwake kutekeleza majukumu fulani, licha ya kiwango cha umuhimu wa majukumu hayo kwake, ima iwe ni jukumu la Kiislamu, la kimaumbile, matamanio au ghariza, uchungaji watoto, faida ya kiuchumi, masomo au hata majukumu madogo madogo ya nyumbani. Ni kana kwamba kuna kizingiti, kinachozuia kufanya jambo na kizingiti hiki hakiwezi kuondolewa na kwamba kwa bahati mbaya nguvu hiyo pia inazuia jukumu hilo maalumu kutotekelezwa. Hali hii ni hali ya uvivu. Mtume Muhammad (saw) alikuwa akipenda kuomba:

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْهَمِّ وَالْحَزَنِ، وَالْعَجْزِ وَالْكَسَلِ، وَالْبُخْلِ وَالْجُبْنِ، وَضَلَعِ الدَّيْنِ، وَغَلَبَةِ الرِّجَالِ»

"Ewe Allah, mimi najilinda kwako kutokana na wasiwasi na huzuni, na ulegevu na uvivu, na ubakhili na uoga, na kuzongwa na madeni, na kughilibiwa na watu."

Uvivu waweza kuwa hatari mno kwa Muislamu na waweza kumvunja moyo kutokana na amali ya Da'wah, ambayo ni wajib na pia muhimu sana katika uhalisia wa leo wa Ummah pasi na Khilafah. Endapo Muislamu atahisi uvivu aina hii kwa amali ya Kiislamu ya kurudisha tena Khilafah au faradhi nyenginezo za Kiislamu, basi anapaswa kustaajabu ni kwa nini yuko katika hali hii na kuwa na hisia hii ya ulegevu.

Kuna baadhi ya tafiti ulimwenguni kuhusu hali hii ya uvivu. Aqliya ya kirasilimali pia huathiriwa na tatizo hili. Kutokana na matatizo ya kiuchumi katika miaka ya nyuma taasisi kadha wa kadha za kisayansi ziliingiwa na hamu ya kutaka kufanya utafiti iwapo uvivu wa wafanyikazi unaathri maendeleo ya kiuchumi au la na nini kinachowapelekea wafanyikazi kuwa wavivu. Tyler Cowen, profesa wa uchumi katika Chuo Kikuu cha George Mason alisema kuwa wafanyikazi wa Kiamerika wamekuwa wavivu na hili linasababisha Amerika kulemaa kiuchumi. Ripoti mpya ya hali ya sehemu za kazi za Kiamerika inakadiria kuwa wafanyikazi wasiojituma huigharimu Amerika kati ya dolari bilioni 450 na 550 kila mwaka kutokana na kupotea kwa uzalishaji.

***Endelea Uk..3***



Email: info@uqab.or.ke

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2015 uliofanywa na Eden Springs uligundua kuwa takriban nusu ya wafanyikazi wa Uingereza wamevunjika moyo na wavivu kazini na utafiti sawa na huu ulifanywa na shirika la bima ya afya la Global health insurance (BUPA) uliotamatisha kuwa asilimia 46% ya wafanyikazi hawatii juhudi ya ziada katika majukumu yao. Kwa kuwa warasilimali wametambua kwamba wafanyikazi wao wamekuwa wavivu katika miaka ya hivi karibuni na kufanya kazi kidogo na ukosefu wa maelewano na kuwa hili huenda likapelekea dosari ya kiuchumi, imewamepelekea kufanya tafiti za ni kwa nini mtu huwa mvivu. Baadhi ya tafiti kuhusu motisha zaashiria kuwa uvivu huenda unasababishwa na kushuka kwa kiwango cha motisha. Kwa warasilimali, inamaanisha kuwa wafanyikazi hufanya kazi vibaya sana kutokana na ukosefu wa motisha na hili hupelekea dosari kwa kampuni. Kwa sisi Waislamu hii yamaanisha kuwa, endapo mtu atakuwa mzembe na mvivu katika utekelezaji wa amali ya Da'wah, itakuwa ni kutokana na ukosefu wa motisha inayompelekea kushindwa kutekeleza jukumu lake la Kiislamu kisawasawa. Hatari kubwa zaidi ya hili ni kuwa inamharibia Akhera yake mwenyewe. Swali linalofuata laweza kuwa, ni wakati gani watu hukosa motisha?

Utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Carnegie Melon ulifichua kwamba watu hukosa motisha pindi wanapoona thamani ndogo katika mapato yanayojitokeza ya kazi zao. Lakini, endapo watu wataweza kuona wazi wazi namna kazi zao zinavyoafikiana na maslahi, malengo na hamu zao, kuna uwezekano mkubwa kwao kuzithamini kazi zao na kupata motisha kuwekeza nguvu zao ndani yake. Hali ya wafanyikazi wa kirasilimali ni kuwa wanadhulumiwa kwa ajili ya maslahi na malengo ya wengine, na hivyo basi inaeleweka kuwa baada ya muda hukosa motisha kazini na hivyo basi kuwa wavivu. Kwetu sisi hii yamaanisha, yakaribiwa kuwa haiwezekani kwa Muislamu anayefanya kazi kwa ajili ya radhi bora za Allah (swt) na kwa ajili ya Akhera, kukosa motisha katika majukumu yake ya Kiislamu na pia katika faradhi ya kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume. Pindi anapoelewa kuwa maisha ni mtihani tu na yanahusu ni nani anayeishi kwa mujibu wa sheria za Allah (swt), basi kimaumbile atawekeza nguvu nyingi na uwezo katika kufikia maslahi, malengo yake na natija ya mwisho.

Vilevile watafiti wa Australia wamegundua hali mpya inayo nasibishwa na uvivu wa hali ya juu: dosari ya upungufu wa motisha (MoDeD). MoDeD hufafanuliwa kama uvivu mkubwa na ulegevu. Vile vile ni ukosefu wa motisha pindi mtu: apotezapo hamu haraka, kutomaliza mambo aliyoyaanza, kuchelewesha na kusitisha kufanya mambo, kujiepusha na kufanya mambo, kulemaa, dhana kuwa yeye ni dhaifu, kuhisi kubanwa, kuhisi kutoeleweka, kuhisi upweke, uchovu na mawazo, kutaka kuimarisha maisha yake, lakini kutofanya lolote kwa hilo, kutokuwa na malengo, au matarajio na kujua kuwa huenda akapata zaidi, lakini hana moyo wa kuzikabili changamoto mpya.

Motisha kwa lugha ya Latin “movere” ni kitu kinachomsukuma mwanadamu kufanya jambo. Motisha ni msukumo wa ndani. Ndio unaokitia nishati kitendo. Kutokana na haya, ikiwa mtu atatambua kwamba amekuwa mvivu katika utekelezaji wake wa majukumu ya Kiislamu pamoja na amali ya Da'wah, anapaswa kuzingatia kama ana motisha ya kutosha kwa majukumu haya. Motisha pekee ya Muislamu ni radhi za Allah (swt) na Pepo ya milele. Hii inamaanisha kuwa daima anapaswa kukumbuka lengo lake ili daima abakie na motisha na daima asonge mbele na ari na ikhlasi na kutimiza majukumu yake ya Kiislamu. Muislamu anapaswa kuwa na fahamu safi za Kiislamu kuhusu maisha haya na kwamba atimize jukumu lake sio kwa kulazimishwa bali kutokana na khiyari yake mwenyewe. Kwa hivyo uwezekano ni mkubwa kwamba fahamu hizi safi zitamsaidia kutopoteza muono wa lengo lake na hivyo hataporomoka ndani ya makucha ya Dunia hii.

Elimu juu ya Jahannam kamwe haituruhusu sisi Waislamu kuwa wavivu na wazembe katika majukumu yetu ya Kiislamu, vile vile hali mbaya ya Ummah haituruhusu kuwa wavivu katika Da'wah ya kulingania Khilafah.

**Amanah Abed**
**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Suluhisho la Matatizo yanayoikumba Sekta ya Elimu halipo katika Uvaaji wa Sare Sawia bali lipo katika Kuiondosha Sera ya Elimu ya Kisekula ya Kikoloni



Wakenya wameachwa njia panda kutokana na kauli kinzani baina ya Viongozi katika Wizara ya Elimu na Muungano wa Wazazi (KPA) nchini Kenya kuhusiana na pendekezo la Muungano wa Wazazi Kenya kuwa wanafunzi wa shule za msingi wote kuvaa sare sawia yenye rangi ya kijivu na shule za upili kuvaa sare sawia yenye rangi ya samawati tofauti ikiwa ni alama ya shule pekee. Mwenyekiti wa Muungano huo, Nicholas Maiyo amesema walitoa mapendekezo hayo kwa Wizara ya Elimu kama wazazi baada ya Warsha ya wiki moja iliyoandaliwa huko Machakos mwanzoni mwa Julai, 2018.

Mapendekezo hayo yaliwekwa wazi na Katibu katika Wizara ya Elimu, Belio Kipsang alipokuwa katika sherehe ya kuadhimisha utekelezaji wa mpango wa kukiboresha kiwanda cha nguo kinachomilikiwa na Chuo Kikuu cha Moi; Jumamosi, 7 Julai 2018. Alisema kwamba, Wizara yake inaifanyiakazi sera itakayojumuisha pendekezo hilo la wazazi. "Pendekezo hilo lilitoka kwa wazazi ambao wamekuwa wakilalamika kutokana na gharama ya juu ya ununuzi wa sare za shule…" akaendelea kusema, "Tunataka kuwalinda watoto wetu dhidi ya wale wanao wanyemelea …" akaongezea "Tunapokaribia kuwa na sare sawia katika shule zetu, tunataka Rivatex kujiandaa ili kuweza kucheza dori katika utengenezaji wa sare zitakazohitajika." Matamshi hayo yalizusha taharuki na gumzo katika mitandao ya kijamii. Siku ya Jumatatu, 10 Julai 2018; Waziri wa Elimu Amina Mohamed alisema kuwa uamuzi wa shule kuvaa sare sawia bado hauja amuliwa rasmi. Akizungumza na vyombo vya habari Jogoo House alitamka "Shule zina wadhamini na hiyo inamaanisha kuwa tuwatake ushauri kabla kufanya maamuzi yoyote."

Kauli hizi zinaashiria wazi kuwa Serikali haijali sekta ya elimu isipokuwa inajali kunyanyua uchumi wake ambao kihalisia ni kwa tabaka dogo la wanasiasa walafi wa kibepari. Uchumi unataka kuboreshwa kupitia Sekta ya Viwanda chini ya madai ya kutimiza ruwaza yake maarufu ya Ajenda Nne Kuu (Big Four Agenda). Kwa mujibu wa taarifa ya sera ya makadirio ya bajeti ya 2018 (2018 Budget Policy Statement) iliyotolewa 19 Januari 2018; serikali inapania kuongeza mgao wa mapato ya sekta ya utengenezaji kutoka asilimia 9 hadi asilimia 15 ya uzalishaji jumla wa taifa (GDP) kufikia mwaka 2022. Kwa upande wa utengenezaji nguo, serikali inalenga kukuza uzalishaji wa pamba

*Endelea Uk..5*

kutumia njia za kisasa, ambazo zitakuwa na uwezo wa kuzalisha mara tatu zaidi na kuwapa motisha wawekezaji kujenga mitambo ya nguo madhubuti. Hivyo kupelekea idadi ya 50,000 ya vijana na wanawake kuweza kuhusishwa na sekta hiyo kupitia mafunzo na hatimaye kiwango cha viwanda vya urefu wa milioni 5 kwa mguu kubuniwa kupitia uzalishaji wa pamba. Kwa kufanya hayo sera hiyo inasema 'Kenya itaongeza mapato kutoka katika sekta ya nguo kutoka bilioni Ksh.3.5 hadi Trilioni Ksh.2, na kutoa nafasi za kazi 500,000 katika kukuza pamba na nafasi za kazi 100,000 katika kutengeneza nguo mpya kufikia mwaka 2022.'

Ni wazi kwamba Muungano wa Wazazi Kenya (KPA) hauna uchungu na hali ya sekta ya elimu kwa kuwa imejisalimisha na kuwa mkono wa serikali katika kuitumikia kufanikisha malengo yake. La msingi ambalo Muungano wa Wazazi Kenya lingekuwa lina washughulisha usiku na mchana ni namna gani wangeliweza kutafuta njia ya kuiondosha sera ya elimu inayotoa dira juu ya elimu ya watoto wao jumla kuanzia chekechea hadi chuo kikuu. Kwa sababu sera ya elimu iliyopo ni ile iliyoasisiwa na mkoloni tangu alipowasili nchini hapa. Nayo ni kuwa Elimu ni ala inayotumika kumakinisha fikra na fahamu za utumwa/kujisalimisha kwa mwanadamu/mkoloni na kufanya vile anavyokuamrisha kwa mujibu wa akili yake inavyomtuma ima umfanyie kazi kiwandani kwake au mahali popote pale. Sera hii imewafanya watoto wakienzi na kutamani kuwa kama wamagharibi wakoloni walio watawala mababu zao. Hili limewapelekea kujisalimisha kikamilifu na kujihisi madhaifu mbele ya maamrisho ya wamagharibi wakoloni wasekula wakirasilimali.

Sera hii iliyoasisiwa juu ya akili finyu ya wakoloni wamagharibi wenye itikadi ya kisekula na mfumo wa kirasilimali haina natija yoyote isipokuwa kuzalisha watumwa wa fikra za kimagharibi zinazopelekea wao kudidimia zaidi ya wanyama kutokana na kuwa fikra hizo ni kinyume na maumbile ya mwanadamu. Mfano mtu ni Professa au Daktari kisha anajienzi kwa kuwa yeye ni 'Shoga'. Hilo ni jambo lakustaajabisha maanake msomi ni yule ambaye jamii inamtegemea katika kuongoza kizazi kijacho kwa kuwa mstari wa mbele katika upeo wa hali ya juu ya ufahamu. Lakini yeye msomi ndiye aliyekuwa duni thamani; Je huyo mwanafunzi wake atakuwa vipi?!

Suluhisho lipo katika Uislamu; mfumo unaotoka kwa Muumba wa Wanadamu na anayetambua lipi zuri na baya kwa viumbe vyake. Uislamu kupitia Dola ya Khilafah iliyosimamishwa kwa njia ya Utume, itikadi ya Kiislamu ndio msingi ambao juu yake imejengwa sera ya elimu. Mtaala wa elimu na mbinu za ufundishaji zote zimeundwa kukinga kupotoka kutokana na msingi huu. Lengo la elimu ni kuzalisha shakhsiyya 'utambulisho' ya Kiislamu katika fikra na tabia, na kuwapa watu mafunzo ya kisayansi na maisha jumla. Kwa hiyo masomo yote katika mtaala wa elimu yatafunzwa kwa mujibu wa msingi huo.

Ama kuhusu suala la uvaaji wa Sare au Sare sawia hilo sio suala nyeti na halitokuwa na mvutano kama inavyoshuhudiwa hivi sasa nchini Kenya kutokana na kuwa kila mmoja anavutia mrengo wake ili aweze kupata bahashishi zaidi kumliko mwenzie. Kwani Dola ya Khilafah kupitia Khalifah mchajiMungu itatoa muongozo rasmi ulio ndani ya mipaka ya Kishari'ah na unaolenga kuwafanyia wepesi raia watakaokuwa wanaishi ndani ya Dola hiyo wakati huo kuhusiana na wanafunzi kuvaa sare au la.

Kwa mara nyingine imedhihirika wazi kuwa itikadi ya Kisekula na mfumo wake wa Kirasilimali unamtizama mwanadamu kama mashine na daima unaomuangalia kwa kipimo cha faida anachotoa au atakavyotumiwa kufikia uzalishaji zaidi wa viwango vya juu vya taifa au hata kutumika kuhalalisha na kuharamisha mipango fiche ya serikali za kikoloni za kisekula.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama Katika Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Nigeria Yakabiliana na Mustakbali Usiothabiti



Tangu uhuru mwaka wa 1960, historia ya kisiasa ya Nigeria imekuwa ya kuzongwa na matatizo kadhaa - vita vya kikabila, vita vya kidini, vita vya mafuta, mapinduzi ya kijeshi nk. Takribani asilimia 75 ya miaka baada ya uhuru ilitumiwa chini ya utawala wa kijeshi na udikteta. Hata hivyo, ghasia za Nigeria hazijawahi kufikia kiwango cha wenzao wa Afrika kama Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR). Nigeria ilikuwa kwenye rada ya wakoloni wa Ulaya kwa karne nyingi. Ilikuwa ni sehemu ya 'Pwani ya Wafungwa' na iliyo barikiwa na rasilimali za madini. Waingereza waliweka waliiteka na kufanya biashara ya utumwa na kusafirisha mafuta ya nazi nje.

Japo, ilipata upinzani kutoka kwa watawala kama wa Sokoto na Mfalme Koko, meli zao za 'Wamisheni' zilichukua udhibiti wa moja kwa moja katika baadhi ya sehemu na njia isiyo ya moja kwa moja katika sehemu nyinginezo. Waingereza walikuja Nigeria na ujumbe wa kueneza Ukristo kwa njia ya Wamishenari. Lakini ukweli nyuma ya 'Umisheni' wake ilikuwa ni ukoloni.

Makubaliano ya dola kuu za kiulimwengu katika kongamano la Berlin (1889-1890) yalianzisha Kinyang'anyiro cha Afrika. Hili liliifanya Afrika kuwa mali ya kibinafsi ya mataifa ya kikoloni. Mfalme Leopold wa Ubelgiji alitangaza makoloni yake kama falme zake za kibinafsi.

Nigeria iligundua mafuta mwaka wa 1956. Hii iliifanya Nigeria kuwa 'Hifadhi' au 'Mamlaka' muhimu na yenye thamani zaidi. Hili pia lilikuja wakati ambapo mizani ya utawala ya kimataifa ilikuwa inagura na mivutano ya kudhibiti maeneo ya mafuta ilikuwa kwa kasi duniani kote. Afrika bado haikuwa sehemu ya uwanja wa siasa za kiulimwengu hadi 1960.

Kwa hivyo, maslahi ya Uingereza hayakukabiliwa na tishio lolote nchini Nigeria mpaka kuibuka kwa Marekani kuwa dola kuu duniani baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Ulaya yote ilitingishwa na vita hivi, kufuatia kumalizwa kwa rasilimali zake na Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia na Mporomoko Mkuu wa kiuchumi wa 1929. Hili liliifanya kuyakamata kwa nguvu zaidi makoloni yake.

*Endelea Uk..7*



Email: info@uqab.or.ke

Marekani iliibuka yenye nguvu kubwa na jeshi lake baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Ilijitokeza kudhibiti ulimwengu baada ya kugundua na kuonja kiasi 'kikubwa' cha mafuta duniani. Kisha ilianza kusaidia harakati za uhuru katika 'Ulimwengu wa Tatu' – Mataifa yaliyo koloniwa. Kwa hiyo, ilifunga mkataba na Nikita Khrushchev, Waziri Mkuu wa Soviet mwaka 1961, ili kugawanya ulimwengu kati ya Marekani na Umoja wa Kisovieti. Hii ndiyo iliyokuwa sababu ya Marekani kuwaruhusu Wakomunisti kuingia sehemu za Afrika na Asia.

Ilhali, 'Uingereza Kuu' ilikuwa inageuka kuwa 'Uingereza Ndogo', Marekani iligundua kwamba ilistahili kuinyang'anya Ulaya makoloni yake ili kuimarisha nafasi yake ya kimataifa. Baada ya kutoa 'uhuru' kwa Makoloni haya, Wakoloni waliwaachia mamlaka vibaraka wao ili kuhifadhi maslahi yao; hii ndiyo iliyokuwa sababu ya mapinduzi na mapinduzi dhidi.

Uingereza iligundua kwamba ilikuwa dhaifu sana kukabiliana na Marekani moja kwa moja, kwa hiyo ilipitisha sera ya Kujihifadhi Kibinafsi (Self-Preservation), ambayo ilifanywa kwa njia mbili: kushirikiana na Marekani na kutibua mipango yake wakati mwingine; ikitaraji kushawishi matokeo ya kisiasa kwa manufaa yake katika hali zote mbili. Kama alivyosema katika nukuu yake maarufu mno; Bwana Henry John Temple, 3rd Viscount Palmerston – Waziri Mkuu wa Uingereza wa wakati huo katika karne ya 19 –'Hatuna washirika wa milele, na hatuna maadui wa kudumu. Maslahi yetu ndiyo ya milele na ya kudumu, na maslahi hayo ni wajibu wetu kuyafuata'. Hii ni taarifa inayo heshimiwa na dola zote za kikoloni.

Licha ya udhaifu wake, Uingereza ni nzuri katika ujanja wa kisiasa. Katika kitabu chake, 'The Post American World', Fareed Zakaria alitoa ufupisho wa Sera ya Kigeni ya Uingereza baada ya Vita vya Pili vya Dunia: 'Picha za Roosevelt, Stalin na Churchill katika kongamano la Yalta mnamo Februari 1945 kwa kiasi fulani zinapotosha. Hakukuwa na 'wakubwa watatu ' huko Yalta. Kulikuwa na 'wakubwa wawili ' pamoja na mjanja mmoja mahiri mfanyi biashara wa kisiasa aliyeweza kujiweka yeye na nchi yake katika mchezo huo, ili Uingereza idumishe vyema mambo mengi ya ufalme mkuu hadi mwishoni mwa karne ya 20.'

Baada ya miaka ya kupanda na kushuka kwa watawala wa kiraia na kijeshi, Marekani hatimaye ilipata mshiko thabiti juu ya Nigeria wakati Olusegun Obasanjo alipochukua utawala mwaka 1999. Marekani ili hakikisha kuwa kibaraka wake alichaguliwa baada ya Obasanjo mpaka uchaguzi wa 2015 wakati kibaraka wa Uingereza kwa muda mrefu, Muhammadu Buhari, alijitokeza huku akitabasamu kutokana na bahati ya kushinda uchaguzi baada ya kugombea kwa miaka mingi. Marekani haikuwa na chaguo kwa sababu ilikosa mtu muaminifu wa kumuunga mkono – kwani Goodluck Jonathan alikuwa ameharibu mipango yake. Kuyachakachua matokeo ya uchaguzi na kumkabidhi ushindi mgombea wake kungechochea ghasia, hasa eneo la Kaskazini – ambalo ni ngome ya Buhari. Marekani kwa hakika hakutaka hilo. Buhari alichukua utawala kwa niaba ya Waingereza. Alikuwa, hata hivyo, akizungukwa na viabaraka wa Marekani; mfano wa Saraki na Kwankwaso.

Marekani inafanya jitihada kubwa za kupata mgombea wa kuaminika. Lakini 2019 hauonekani kama mwaka wa yeye kuitia mikononi tena Nigeria. Mgombea anayetarajiwa zaidi, Atiku Abubakar, ana hadhi duni machoni mwa watu wa Nigeria – hasa eneo la Kaskazini lenye wakaazi wengi ambapo Buhari anaungwa mkono kiupofu. Gavana wa zamani wa Kano, Kwankwaso, huenda akawa chaguo bora zaidi.

Tatizo la Nigeria lilisababishwa na ulafi wa Ukoloni wa Kimagharibi. Historia ya kisiasa ya Nigeria daima imekuwa ni hadithi ya mapambano ya kikoloni.

Kwa hiyo, uchaguzi wa 2019 ni mapambano kati ya dola za Kikoloni – nchini Nigeria, ni Marekani na Uingereza. Nigeria ni lazima ijikomboe kutokana na minyororo ya Ukoloni na inapaswa kubeba fikra safi yenye natija kwa binadamu ili kupata maemstsndeleo ya kikweli.

**Umar Abu Ammar Bin Ahmad**
**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Sakata ya Sukari ni Usimamizi Mbaya wa Serikali za Kibepari




Kashfa ya sukari imekua ikiendelea kuleta mikwaruzano katika utawala wa Jubilee baina baina ya Rais Uhuru Kenyatta na makamu wake William Samoe Ruto. Wandani wa kisiasa wa Ruto wakiitaja kuwa ni yenye malengo ya kuwahujumu kisiasa. Sakata hii iliibuka pale kulipopatikana tani milioni 1.2 katika baadhi ya maeneo ya Kitui, Machakos na Nairobi. Sukari hii inatajwa kuingizwa nchini kimagendo. Kilichochachawiza zaidi ni madai ya kuwa sukari hii pia imechanganywa ndani yake na madini ya zebaki (mercury). Ili kufahamu nyuma ya sakata hii, ni vyema kutaja kwanza matukio yafuatayo:

**Kwanza:** Utafiti uliofanywa na taasisi kuu ya wanafikra huko Denmark (Denish Think Tank) ulitaja kwamba kuna takribani ya wafanyibiashara 70 wakiwemo vigogo wa kisiasa katika miji ya Kismayu, Garissa na Nairobi wanaohusika na biashara ya kimagendo ya sukari inayowatilia mamilioni ya dolari za Marekani. Sukari inayotumiwa hapa Kenya nyingi inaaminika kuingizwa nchini kinyume cha sheria kutoka Brazil.

**Pili:** Mwaka 2014 malori 230 yalikuwa yakiondoka Kismayu kila wiki huku kila moja likibeba tani 14 za sukari. Al-Ashabab licha ya kukosa udhibiti wa bandari ya Kismayu walikuwa wakitoza kila lori lilikuwa kitita cha $ 100 (Ksh 100,000).

**Tatu :** Kulingana na ripoti ya Journalists For Justice Lobby group iliyochapishwa mwaka 2015, ilisema kuwa mwaka 2014 tani 150,000 za sukari ziliingizwa kinyume cha sheria nchini Kenya kutoka Kismayu. Tani hizi zilikuwa ni sawa na $400 milioni (Ksh 40billion). Mapato haya inadaiwa yamekuwa yakigawanywa baina ya KDF, Al-Shabab, wafanyibiashara wa humu nchini, wanasiasa polisi pamoja na maofisaa wa Mamlaka ya ushuru ya Kenya (KRA). Ripoti hiyo iliyochapishwa kwenye gazeti la **Sunday Nation tarehe 1 Julai 2018**, ilitaja kuwa Al-shabab na KDF wamekuwa wakigawanyiana maeneo hayo ya vituo vya kiukaguzi wa barabarani kutoka Kismayu hadi mpakani mwa Kenya. Inaendelea kusema kuwa ; KDF pamoja na maofisaa wa Somalia huko Jubaland wamekuwa wakitoza ushuru wa $2 Ksh(200) kwa kila gunia la sukari la kilo 50 ama kwa wakati mwengine kilo 100.Kwa upande wa Somalia eneo la mpakani la Dhobley utawala wa Jubaland umekuwa ukitoza ushuru wa $600 kwa kila lori. Na wamiliki wa malori haya wamekuwa wakiwalipa KDF $600 katika mpaka wa Liboi ili waruhusiwe kuingia na kulipa $600 nyengine kwa polisi katika kambi ya wakimbizi ya Dadaab.

**Nne:**Tarehe 19 June,2018 Kiongozi wa waliowengi Bungeni Adan Duale alimshtumu waziri wa fedha Henry Rotich na mwenzake wa usalama wa ndani Fred Matiang'i kwa kuwahami baadhi ya matajiri wanaohusika na uingizaji wa sukari isiyo bora kwa matumizi ya wanadamu. Duale alitaja kampuni 100 alizodai kuwa zinahusika na uingizaji wa sukari yenye sumu yenye thamani ya shilingi bilioni 39.2. Naye mbunge wa Aldai; Cornelly Serem alimtaja Muhoho kakake Uhuru Kenyatta kwamba anahusika kwenye sakata hii.

**Tano:** Kulitoka kauli zinazokinzana za mawaziri wawili serekalini; waziri wa viwanda Adan Mohammed akikanusha madai ya kuwepo kwa zebaki ndani ya skari huku Fred Matiang'i akitaja kuwa sukari ina sumu!

*Endelea Uk..9*

**Sita:** Matumizi ya sukari nchini Kenya yamekua yakiongezeka na kwa upande mwengine uzalishaji umekua ukishuka. Kwa mfano mwaka 2014 uzalishaji wa sukari ulikuwa ukikimu asilimia 70 ya matumizi ya ndani ya nchi. Miaka minne baadaye yaani mwaka 2018 uzalishaji huu ulikua tayari hauwezi kukimu matumizi ya sukari kwa asilimia 62. Mwaka 2014 tayari Kenya ilikuwa na uhaba wa bidhaa hii wa tani 200,000.

**Saba:** Sekta ya uzalishaji sukari kama sekta nyingine imekuwa ikikumbwa na ufisadi wa washikadau wake…huku mabwenye kwa makusudi wakiuwa viwanda vya humu nchini wakisingizia kuvifanyia marekebisho! Wakulima wa miwa nao wakinyimwa malipo yao ya miezi kadhaa. Haya yakifanyika wafanyabiashara wamekuwa wakiagiza sukari kutoka mataifa kama vile Brazil. Hali hii imepelekea sukari inayozalishwa nchini kuwa ghali mno kuliko inayoletwa kimagendo.

Uhalisia uliopo hapo juu una thibitisha kuwa;

Ni wazi kuwa biashara ya sukari ni yenye kutekwa na wanasiasa wakorofi serikalini wanaodhimiti uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hii muhimu. Na hao ndio wanao sababisha tatizo hili kwa hesabu za tamaa zao za kibepari. Hivyo Sakata ya sukari ni ya kutengenezwa 'Artificial' wala sio kweli kuwa Kenya ina uhaba wa sukari au inahitaji sukari kutoka nje. Ikimbukwe pia kuna kashfa ya mahindi nayo inafuata mkondo huo huo. Ama kuwa sakata hii inafuata mkondo wa kisiasa hili linaashiria kuwa wanasiasa wote ni wafisadi na wanajuana hivyo hutegemea nani atakua mhodari kuona ufisadi wa mwenzie na kuitumia vyema fursa ya kumhujumu mpinzani wake kisiasa. Isitoshe pesa zinazotokamana na sukari hutumiwa na wanasiasa katika kuendesha kampeni zao za kisiasa. La kuzingatia hapa ni kuwa tume za kuhoji na za 'kupambana' na ufisadi zote hizo si lolote bali kama sarakasi tu bali tume hizo zenyewe huajiriwa na hao wafisadi! Fauka ya haya Urasilimali wenyewe ni ufisadi hivyo serikali au taasisi za kirasilimali kamwe hazitarajiwi kuondosha jinamizi hili.

Serikali za kibepari kushindwa katika kulinda viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa muhimu kwa raia wake. Aidha tawala hizi zinashindwa katika kusimamia biashara za nje. Na hii ni khiyana ya kiuongozi kwani kiongozi ni yule anaye takikana kutanguliza maslahi ya raia wake zaidi hata kuliko maslahi yake yeye.

Uislamu kwa upande wake una angalia biashara kwa mtazamo maalumu unaopelekea maslahi kwa raia wake. Biashara inayofanyika baina ya raia ndani ya utawala wa Kiislamu asili yake ni halali na kila raia ana haki ya kuuza na kununua muhimu kinachouzwa ni halali. Serikali kwa upande wake haifai kuingilia katika biashara za raia wake bali kwa upande wake inatakikana kuwa na usimamizi tu wa kijumla yaani kuhakikisha kuwa raia wake wanajifunga na sheria katika biashara zao.

Haifai Kiislamu kuzuia raia kufanya biashara na raia wa mataifa mengine isipokuwa biashara hii ya nje hulazimika kusimamiwa na serikali kwa sababu huingia ndani yake mahusiano baina ya dola moja hadi nyingine. Kwa mfano serikali inaweza kuzuia mauzo ya bidhaa za nchi katika taifa jengine huku pia yaweza ikaruhusu mauzo ya baadhi ya bidhaa. Wafanyibiashara nao huangaliwa yaani wale wanaoagiza bidhaa nje au kuuza nje je ni raia wa mataifa ambayo yanatakikana kupigwa vita au la.

Ni jukumu la serikali kuhakisha hakuna uhaba wa bidhaa muhimu kama vile sukari na ikitokea uhaba huu serikali yafaa ichunguze chanzo chake na kutatua mara moja. Kwa mfano ikitokea ni uzembe na utepetevu wa washika dau basi hatua za haraka kuwauzulu yafaa kuchukuliwa. Aidha, serikali pia huwajibika kwa kupeana mikopo kwa wakulima bali kuwawezesha ili waweza kulima kilimo cha kujitosheleza na pia biashara.

Ama suala la kuwa na sumu ndani ya sukari, hili suala ni moja wapo ya ukatili wa mfumo wa kibepari na makampuni yake. La kuzingatia ni kuwa vyakula vingi leo vilivyomo sokoni viko viwango vya chini sana kiafya. Mafuta ya kupikia, Unga, Mchele hata gesi bidhaa zote hizi mara nyingi haziko kwenye kiwango kizuri kwa matumizi ya wanadamu. Hili ni jambo linalofanywa kimakusudi kwa zilezile tamaa za kibepari za kujiongezea mapato kwa njia za mkato. Na hii ndio maana makampuni mengi yameshtumiwa kuwa kazi ya kutengeza bidhaa ghushi. Janga hili Uislamu umelitatua kwa kumuwajibisha kiongozi kuangalia masuala yanayowazunguka raia wake ikiwemo hili kwa kuwa yeye ndiye mchungaji. Uislamu ukaweka hakimu maalumu kwa jina la Muhtasib ambaye huyu hana ofisi maalumu bali yeye ofisi yake ni pale tu anapoona uhalifu wowote unaopelekea madhara kwa raia kama uuzaji wa bidhaa ghushi hapo hapo anatoa hukumu. Hivyo sokoni, barabarani na nyumbani anatakiwa kutoa hukumu zake kwani hahitaji kiongozi wa mashtaka wala mlalamishi bali pindi atakopoona uvunjwaji wa haki yoyote ile anatoa hukumu yake kwa mujibu wa Shari'ah.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari, Hizb ut Tahrir Kenya**

# Marekani Inapaswa Kujifunza Kutokana na Uhuru wake



Tarehe 4 Julai ya kila mwaka Marekani huadhimisha siku ya kumbukumbu ya uhuru iliyoupata kutoka kwa Uingereza mwaka 1776. Uhuru huo ulipatikaniwa baada ya mashaka, madhila na muhanga wa hali ya juu, kitu ambacho bila ya shaka yoyote kiligharimu maisha ya wamarekani kwa maelfu kama si malaki. Tukio la uhuru wa Marekani ni tukio kubwa lililopelekea kuzaliwa kwa dola kubwa, yenye nguvu baada ya kuung'oa ukandamizaji uliootа mizizi na dhulma iliyokita muda mrefu kutoka kwa wakoloni wa kiengereza.

Marekani ilitawaliwa chini ya makucha ya ukoloni kwa karibu miaka 150 kwa mkono wa chuma ikiwa chini ya tawala ya kikoloni katika majimbo yake mbali mbali, hali iliyopelekea kupita katika kipindi kigumu katika historia yake. Katika kipindi chote hicho ilikabiliwa na mkondo wa kubanwa, mateso, ukandamizaji ikiwemo wananchi wake hata kutoruhusiwa kupiga kura kuchagua viongozi wanaosimamia mambo yao, kutozwa kodi kubwa, vikwazo katika biashara na kuporwa rasilmali zake kwa maslahi ya mabepari na makampuni ya kiengereza. Hali hiyo ilishitadi zaidi chini ya utawala wa kidhalimu wa mfalme wa kiengereza George III.

Hatimaye ndani ya karne ya 18 mchakato wa harakati za kutaka kujikomboa na madhila ya ukoloni zilianza kuota mizizi na kushamiri katika nyoyo za wamarekani, na wimbi zaidi la upinzani dhidi ya ukoloni lilionekana waziwazi na kuungwa mkono na wamarekani wengi.

Vuguvugu hili la upinzani lilichukua sura pana zaidi katika mwaka wa 1773 katika jimbo la Boston wakati wamarekani walipoamua kufa na kupona kuitosa majini shehena kubwa ya majani ya chai ya kampuni ya Uingereza waliyokuwa wakiipakua kutoka melini katika bandari ya Boston. Jambo hili lilipelekea kuzuka na kupata msukumo mpya wa kupigania haki zao na kuudai uhuru wao moja kwa moja. Uingereza ilijibu na kukabiliana na vuguvugu hilo haraka sana kwa vitisho na kutunga sheria ya shehena (Intolerable Acts) kwa lengo la kuzima kwa haraka kile walichokiona kuwa ni ' tishio dhidi ya Utawala wa Mfalme'.

Hata hivyo, pamoja na hatua hizo za Dola ya Himaya ya Uingereza, wamarekani walijfunga kibwebwe, hawakuvunjika moyo wala kurudi nyuma katika mchakato wao wa kupigania uhuru wao kwa ushujaa na ujasiri mkubwa wakaendelea na mapambano yao hadi kupelekea kuibuka rasmi vita vya moto vya awali vinavyoitwa 'Bunker Hill' katika jimbo la Massachusetts katika mwaka 1775.

Chini ya Jemadari George Washington na kwa msaada wa dola za Spain na Ufaransa, wamarekani wakaweza katika vita hivi kuibuka washindi, na haraka sana katika mwezi wa Julai, 1776 Kongamano la wamarekani wanaowakilisha makoloni/majimbo 13 (states) walikutana rasmi kutangaza 'Tamko la Uhuru' lililoandaliwa na jopo lililokuwa chini ya Thomas Jefferson na Benjamin Franklin.

*Endelea Uk..11*

Tamko hili liliweka bayana, wazi na moja kwa moja kwamba kuanzia sasa majimbo yao yako huru na wamejifungua moja kwa moja na minyororo ya utawala wa Uingereza. Wamarekani walithubutu kuchukua hatua ya kutangaza uhuru wao kwa ujasiri na ushujaa huku wakielewa wazi kabisa kwamba kutokana na haiba, hadhi, maguvu na mamlaka ya dola kubwa ya Uingereza ulimwenguni na zaidi umuhimu wa koloni la Marekani kwa dola hiyo, kamwe hawatokuwa tayari kuutambua uhuru huo walioutangaza, lakini wamarekani hawakurudi nyuma walisimama kidete na imara katika msimamo wao huo.

Katika mwaka uliofuata Dola ya Himaya ya Uingereza ilishindwa vibaya katika medani ya vita dhidi ya wapigania uhuru. Na kwa fedheha na idhilali ikasalimu amri na kuweka silaha chini katika maeneo ya Saragota na Yorktown. Hata hivyo, na kama ilivyotarajiwa pamoja na 'Tangazo la Uhuru' lililotolewa na Kongamano la Majimbo 13 ya Marekani na kushindwa vibaya kwa Uingereza kwa fedheha katika medani ya vita, bado Uingereza kwa kiburi chake na kudanganywa na maguvu ya dola yake ilichukua karibu miaka saba kulitambua rasmi 'Tamko la Uhuru'. Ilikuwa ni katika mwaka wa 1783 ndipo rasmi Uingereza ilipolazimika kwani haikuwa na namna ila kuutambua uhuru wa Marekani kiukamilifu chini ya mkataba wa Paris (Paris Treaty).

Baada ya uhuru huu wa Marekani iliyoupata kwa tabu, mashaka na gharama kubwa ya muhanga, Marekani ilibidi ikabiliane na changamoto mbalimbali kama vita vya wao kwa wao (American Civil War), kuunganisha majimbo (states) mengine hadi kufikia 50, kujitosa katika uwanja wa mvutano wa kimataifa vikiwemo vita vikuu viwili na kufanya kazi kwa kujituma hatimaye dola hii kufikia hapa ilipo leo.

Kwa bahati mbaya na katika hali ya mshangao, wakati Marekani kila mwaka inaadhimisha siku ya uhuru wake, bado imekosa kujifunza kutokana na tukio hili kubwa katika historia yake ambalo kila mwaka inaliadhimisha. Marekani kwa ghururi inajisahaulisha historia yake, inadharau na kuitupilia mbali na haichukui funzo kutoka katika historia ya harakati zake za kupigania uhuru hususan katika maeneo manne makubwa: -

**Awali,** ikiwa Marekani ilifika mahala baada ya dhulma kupigana na Uingereza ili kutafuta uhuru wake. Na baada ya uhuru wakafanya bidii kwa gharama kubwa kuunganisha nchi yao, kwa kupitia 'Tamko la Monroe' (Monroe Doctrine) wakakataa katakata na wakazipinga hata nchi za Ulaya kuingilia mambo yao, si tu katika nchi yao bali katika bara lote la Marekani.

Vipi leo Marekani inalisahau hili kwa kuzifanya nchi za wengine kama mazizi yao ya ng'ombe kwa kuwaingilia na kuwalazimisha mambo kinyume na matakwa ya nchi hizo na kuwafanya viongozi na raia wa nchi hizo kama watumishi wao kama si watumwa kamwe?

**Pili,** Marekani lazima itanabahi kwamba mabavu na kiburi cha dola kamwe si dalili ya nguvu ya dola, bali katika mazingira fulani ni sababu ya maangamizi yake. Marekani ichukue funzo kuwa wakati wa kuanza kwa vuguvugu la 'makoloni' ya kimarekani kudai uhuru wao kutoka kwa Uingereza, baadhi ya watu makini katika Dola ya Himaya ya Uingereza kama Edmund Burke waliwahi kuishauri serikali ya Mfalme wa Uingereza kuacha kuchukua hatua za kimabavu dhidi ya makoloni yake ya Kimarekani. Lakini kwa kiburi, majigambo na majivuno ya Mfalme George III pamoja na baadhi ya mawaziri wake waliukataa ushauri huo. Hatima yake ikawa fedheha na idhilali kwa Dola ya Himaya ya Uingereza.

**Tatu,** ikumbukwe kuingia kwa Spain na Ufaransa katika mchakato wa kuwasaidia wamarekani kupigania uhuru kulisukumwa na suala moja tu la kimaslahi. Wakiwa na lengo la kuondosha athari ya Uingereza ndani ya makoloni hayo ili madola yao wajenge ushawishi baada yake. Hii ina maana kwamba madola yote ya kibepari huangalia kitu kimoja tu nacho ni 'maslahi' na kamwe si marafiki wa kutegemea. Kwa hivyo, hata leo lau itasimama dola nyengine kubwa, yenye nguvu na rasilmali kwa kutumia kipimo cha maslahi upo uwezekano mkubwa baadhi ya madola ya magharibi ambayo Marekani inayachukulia kuwa marafiki zake wa karibu kumuacha mkono na kuiunga mkono dola mpya iliyosimama kwa kutaraji kupata maslahi zaidi kutoka dola hiyo kuliko wanayoyapata kutoka kwa Marekani. Kwa kuwa katika mfumo wa ubepari 'hakuna urafiki wa kudumu kuna maslahi ya kudumu'. Na kwa hilo pia ni rahisi kwa madola hayo kugombanishwa baina yao kwa ajenda ya maslahi.

**Nne,** Marekani inafaa pia ijifunze kwamba msukumo uliowafanya watu wao kujitoa muhanga kupigania uhuru wao ni ile hali ya kimaumbile aliyonayo kila mwanadamu, hali ya kuwa na hisia ya kutaka kuishi na kuendeleza maisha yake' (survival instinct). Kwa hisia hii wanadamu wote hutaka na kupenda waishi katika maisha ya furaha, amani na utulivu wakiwa huru kujiendeshea mambo yao wenyewe kadri inavyowezekana. Na inapotokezea kukosekaniwa jambo hilo, kutokana na ukandamizaji au dhulma, mwanadamu huyu hufika mahala akaamua kuondosha dhulma hiyo ili ajiletee maisha mazuri na ya furaha kwa gharama yoyote kwa kuwa huo ni msukumo wa kimaumbile.

Kwa bahati mbaya Marekani inajitia upofu na kudharau kuchukua mafunzo hayo kutoka ndani ya historia yake na badala yake inaitupilia mbali kwa kuibakisha historia yake kuwa 'nadharia' tu bila ya kuibeba kama dira kwa maisha yao.

**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut Tahrir Tanzania**

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 15: Kujitambulisha Mtume (saw) kwa Banu Shaiban

Katika Halaqa hii tutaangalia ujitambulisha Mtume (saw) kwa Banu Shaiban.

Hakika kujitambulisha Mtume (saw) kwa makabila ili wamnusuru na wamhami ili aweze kufikisha risala/ ujumbe wa mola wake, ni amri kutoka kwa Mola wake, na ni sehemu muhimu ambayo haiwezi kutenganishwa na twariqa/njia ya kisheria ya kusimamisha Dola ya Kiislamu.

Na hiyo si rai ya Mtume (saw) bali ni amri ya Mwenyezi Mungu (swt) iliyopangiliwa na sheria na kuja kupitia Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt). Kwa hiyo ni hukmu ya kisheria na inapasa kujilazimisha nayo kama alivyojilazimisha kwayo Mtume (saw).

Ametoa Abu Naim kutoka kwa ibn Abbas (ra) kutoka kwa Ali ibn Abi Twalib (ra) asema: Allah alipomuamrisha Mtume wake (saw) ajitambulishe kwa makabila ya Waarabu, alitoka nami na Abubakar (ra) mpaka tukafika Mina, tukafika katika kikao cha Waarabu akatangulia Abubakar akasalimia, na alikuwa Abubakar kila mara anatangulia, alikuwa ni mtu mwenye nasaba akasema: Nyinyi ni kaumu gani? Wakasema: sisi ni wa Rabi'ah, akasema: Nyinyi ni Rabi'ah gani? Akaelezea Hadith kwa urefu na katika hiyo Hadith akasema: Kisha nikafika katika mkao wenye utulivu, akatangulia Abubakar akasalimia, asema Ali: Na alikuwa akitangulia kila mara, akawaambia Abubakar: Nyinyi ni kaumu gani? Wakasema: Sisi ni Banu Shaiban bin Tha'labah, akamgeukia Mtume (saw) akasema: Bi abiy anta wa ummiy (kiapo) Hamna watu katika kaumu hii wenye izza zaidi ya hawa...!

Na katika kaumu kulikuwa na Hanii bin Qusayyi, na Muthanna bin Haritha, na Mafruq bin Amr, na Nuuman bin Sharik, akataja Hadith kwa urefu wake mpaka akasema: akasema Rasul (saw) : "Nawalingania kwa shahada ya kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake hana mshirika, na hakika Muhammad ni Mjumbe wa Allah, Na mnipe makaazi na mninusuru na kunihifadhi mpaka niweze kutekeleza aliyoniamrisha Allah (swt)." Hakika Maqureysh walikataa amri ya Allah, na wakamkadhibisha Mtume wake, wakajitosheleza na batili kuliko haki, na Allah ndiye aliyetoshelezeka zaidi na Mwenye sifa. Wakasema: "Sisi tuko katika mkataba tuliofunga na Kisra, ya kwamba tusizungumze na mgeni wala kumkaribisha mgeni, na huenda jambo hili likawa ni katika mambo yanayowaudhi wafalme...! Ukitaka tukunusuru upande wa Waarbu tutalifanya hilo."

Akasema Rasulullah (saw): "Hamkujibu vibaya mlipoweza kusema ukweli...! Wallahi hakuna anayeweza kusimamisha Dini ya Allah ila aliyezunguka pande zote"

Haijuzu kuusoma Mustaqbali (mambo yatakavyokuwa mbeleni) kwa kupitia waqia (uhalisia) wanaoishi nao wabebaji Da'wah. Kisha akasema Rasul (saw) kuwaambia Bani Shaiban: "Je, mwaonaje hamtokaa ila muda mchache Allah atawatunuku miji yao na mali yao, na kuwachukua mabinti zao, je mtamsabihi Allah na kumtakasa?!"
Nu'man bin Sharik akamwambia Mtume: "Hakika hilo ni lako wewe ewe ndugu wa kiquraysh...!"

Kisha Mtume (saw) akasoma:

وَدَاعِياً إِلَى اللهِ بِإِذْنِهِ وَسِرَاجاً مُنِيْراً

"Na mwitaji kumwendea Mwenyezi Mungu kwa idhini yake, na taa yenye kutoa nuru."
[Al-Ahzaab: 46].

Kisha akasimama Rasul (saw) akiwa amemshika mkono Abubakar (ra)...!

Katika Hadithi hii tukufu anatufundisha Mtume (saw) na anawafundisha wabebaji Da'wah darasa lilio na umuhimu mkubwa, nayo ni kuwa haifai kusoma mustaqbali kupitia waqia (uhalisia) wanaoishi nao wabebaji da'wah. Kwani nguvu za batili kiasi chochote zitakavyokuwa kubwa haziwezi kuwarudisha nyuma na ufanyaji kazi ya kuing'oa kutoka mizizi yake na kuiondosha kabisa...! Na nguvu za batili kiasi zitakavyokuwa kubwa mwisho wake ni kupenduka...! Na haikuwa kwa wabebaji ulinganizi ila wazidi thiqa kwa Nusra ya Allah, Na wasubiri mpaka itakapofika ahadi ya Allah...!

**Itaendelea katika UQAB Toleo 19…In Shaa Allah.**

# SWALI/JAWABU: Kongamano la Maraisi Baina ya Amerika na Korea Kaskazini



**Swali:**

Kongamano la maraisi baina ya Amerika Kaskazini na Korea Kaskazini lilifanywa kupitia mkutano wa Maraisi wawili, Trump na Kim mnamo 12/6/2018 nchini Singapore. Walitia saini waraka kwa pamoja mwishoni mwa kongamano hilo. Makubaliano hayo yalifanywa kwa haraka, ikizingatiwa kuwa mzozo kati yao ulifikia kilele mwaka jana ambapo kila mmoja wao alitishia kumpiga mwengine kwa silaha za kinuklia. Ni vipi makubaliano haya yalifanyika kwa haraka? Ni yapi yaliyomo ndani yake na ni zipi natija zake?

**Jibu:**

Ili kuweza kufahamu ukweli wa jambo hili, twapiga darubini yafuatayo:

1- Amerika imejaribu mara kwa mara pamoja na vitisho kuifanya Korea Kaskazini kuachana na silaha zake za kinuklia, lakini vitisho hivi vimeambulia patupu, na Korea Kaskazini haikusalimu amri na wala haikuachana na mradi wake na silaha za kinuklia. Amerika ikaamua kutumia mbinu nyengine, ikiwemo mbinu ya kisiasa na ya kidiplomasia na shinikizo za kiuchumi. Mojawapo ya mbinu hizo ilikuwa ni Amerika kutia juhudi kuifanya China iishinikize Korea Kaskazini. Tulitaja katika Jibu la Swali la tarehe 23/4/2017: Kwa sasabu ya yote yaliyo juu, Amerika kwa sasa haiko tayari kwa vita nchini Korea Kaskazini, na hana masuluhisho mengine muwafaka. Inasubiri China kuishinikiza Korea Kaskazini, na inajaribu kuliharakisha hili, na taarifa zake kwamba Amerika iko tayari kusuluhisha tatizo hilo kipeke yake (yaani, bila ya China) zinaongezeka, kana kwamba inaitishia China kutii Amerika na kuishinikiza Pyongyang kuachana na silaha zake za kinuklia. Amerika imetangaza kupitia Naibu wa Waziri wa Kigeni wa Maswala ya Asia Mashariki na Pacific, Susan Thornton, aliyesema nchi yake haitafuti mzozo na Korea Kaskazini au kuibadilisha serikali yake: “Amerika imeeleza wazi wazi kuwa inataka kutatua tatizo hili na Korea Kaskazini kupitia kuachana na silaha za kinuklia kwa amani katika bara la Korea, kwa yakini hatulengi mzozo au kubadilisha serikali.” (Chanzo: Russia Today, 17/4/2017). Mawasiliano ya kidiplomasia baina ya pande mbili hizi yalianza kupitia China. Shinikizo zimewekwa kupitia kulazimisha vikwazo vya kiuchumi na kugomewa kisiasa kwa ili kuitenga kimataifa na kunyanyua propaganda dhidi yake ili kuwalazimisha kujisalimisha na kujitayarisha kuachana na silaha hizo. Iliongeza pia vivutio na ahadi za kukua kwa uchumi moja kwa moja na kupitia Korea Kusini, ambayo imeanza kuungana na Korea Kaskazini na kimataifa wazi wazi kwa ajili yake.

2- Mawasiliano ya siri ya kidiplomasia yalianza kupitia China, ambapo aliyekuwa Waziri wa Kigeni Tillerson aliwasiliana na watu wa Korea Kaskazini kupitia China mnamo Julai 2017. Alielezea upinzani wake kwa mbinu ovyo ya Trump, iliyohatarisha kuiangamiza Korea Kaskazini kutoka katika uso wa dunia, huku Tillerson akifanya maongezi ya kisiri na watu wa Korea Kaskazini nchini China! Wenyeji wa Korea Kaskazini waliposikia vitisho vya Trump walijiondoa kutoka katika mazungumzo hayo na kuondoka nchini China kurudi nchini kwao… Tillerson alikasirika na kumwita Raisi wake bwege mnamo 20/7/2017 kama ilivyo fichuliwa baadaye na shirika la habari la Amerika la NBC mnamo 4/10/2017 lilipowanukuu

*Endelea Uk..14*

maafisa wa tatu wa Amerika. Trump aliandika katika mtandao wake wa Twitter siku moja baada ya Tillerson kutangaza kuwa Amerika ina njia za moja kwa moja za mawasiliano na Korea Kaskazini: "Nilimwambia Rex Tillerson, Waziri wetu adhimu wa Kigeni, kuwa anapoteza muda wake kujaribu kujadiliana na mtu mwenye kombora dogo". Hayo hayo ndiyo yaliyotokea, yaani matumizi ya vitisho wakati wa mazungumzo pindi Makamu wa Raisi wa Amerika Mike Pence alipo jaribu kukutana na watu wa Korea Kaskazini nchini Korea Kusini alipoizuru kwa kisingizio cha kushiriki katika michezo ya Olimpiki ya Msimu wa Baridi. Alikuwa akijitayarisha kwa hilo pindi aliposema mnamo 7/2/2018, alipokuwa akiyahutubua majeshi ya Amerika yaliyoko katika kambi ya wanahewa ya Yokota nchini Japan "Daima tutatafuta amani. Daima tutajikakamua kwa ajili ya mustakbali bora…" (Chanzo: Reuters, 7/2/2018). Alisema haya wakati alipokuwa akijitayarisha kwenda Korea Kusini katika jaribio la kukutana na maafisa wa Korea Kaskazini chini ya kisingizio cha kuhudhuria ufunguzi wa michezo ya Olimpiki ya msimu wa baridi mjini Pyeong Chang, ulio na umbali wa takriban 80 Km kutoka mpaka wa Korea Kaskazini… Lakini Pence siku tatu baadaye mnamo 10/2/2018 alisema: "Hakuna mwangaza kati ya Amerika, Jamhuri ya Korea na Japan juu ya haja ya kuendelea kuitenga Korea Kaskazini kiuchumi na kidiplomasia hadi iachane na mradi wao wa kinuklia na mizinga aina ya ballistic," (Chanzo: Al Arabiya, 10/2/2018). Hii ilipelekea Korea Kaskazini kufutilia mbali mkutano wake na Pence, yote haya yakiashiria kuwa mbinu ya kisiasa ya Kiamerika iliyo tabanniwa na Trump ni kutumia vitisho kumshinikiza mpinzani huyu wakati wa mazungumzo na mawasiliano ya kidiplomasia ili kumfanya mpinzani huyu ajisalimishe kwa yale Amerika iyatakayo. Haya pia yanathibitishwa na Mike Pompeo wakati wa kipindi chake kama mkuu ya shirika la ujasusi la Kiamerika la CIA: "Raisi ana nia ya kutoa suluhisho kupitia mbinu za kidiplomasia… Sisi pia, wakati huo huo, tunahakikisha kuwa tukitamatisha hilo halitawezekana, kwamba tunawasilisha kwa Raisi machaguo kadha wa kadha yanayoweza kufikia nia aliyoitaja", (Chanzo: Reuters, 23/1/2018), na hivyo basi suluhisho la kidiplomasia linajumuisha machaguo mengine yanayoashiria vitisho. Inaonekana kuwa mbinu hii, vitisho wakati wa mazungumzo ya kidiplomasia, haikumfurahisha Tillerson kwa sababu ilimfedhehesha kama Waziri wa Kigeni, na hivyo basi Trump akamtimua…

3- Kwa hiyo mbinu hii haikufanya kazi kwa Korea Kaskazini, na wangesitisha majadiliano kulipokuwa na vitisho vya aina yoyote. Lau kama China haingeingilia kati, kongamano hilo lisingefanyika, hii ndio sababu Trump kufuatia kongamano na Kim wakati wa mkutano wake na waandishi habari nchini Singapore alisema, "Anamshukuru Raisi wa China Xi Jinping, kwa juhudi zake za miezi ya hivi karibuni kuwezesha kufanyika kwa kongamano hili la kihistoria" (Chanzo: AFP, 12/6/2018). China imeishinikiza Korea Kaskazini kulegeza msimamo. "Kiongozi wa Korea Kaskazini Kim Jong-un alifanya ziara isiyokuwa rasmi nchini China kuanzia Jumapili (25/3/2018) hadi Jumatano (28/3/2018)", shirika rasmi la habari la Xinhua liliripoti mnamo Machi 28, ambapo lilijadili kwa kina hali ulimwenguni na bara la Korea, na Raisi wa China Xi Jinping aliwambia mwenzake wa Korea Kaskazini kwamba China imejitolea katika lengo la kuachana na silaha za kinuklia katika bara la Korea na kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu pamoja na kulitatua tatizo hili kupitia mazungumzo na majadiliano. Shirika hili la habari la Korea Kaskazini liliripoti "kiongozi wake Kim Jong-un alizuru China kumpongeza kibinafsi Xi Jinping kwa tukio la kuchaguliwa tena kama raisi wa China kwa kuambatana na tamaduni za kirafiki baina ya nchi mbili hizi…" na "alionesha matumaini kuwa ziara yake nchini China itachangia kumakinika kwa amani na utulivu katika bara la Korea, akitangaza kuwa yuko tayari kwa mazungumzo na Amerika na Korea Kusini pamoja na kufanya mikutano na viongozi wao", na akaongeza: "Kuachana na silaha za kinuklia nchini Korea kunawezekana ikiwa Washington na Seoul zitachukua hatua imara na za pamoja za kufikia amani". Hii ndio maana Trump alitangaza katika mtandao wake wa Twitter mnamo 28/3/2018 furaha yake ya kile kilicho patikana kutokana na ziara hiyo: "Nilipokea ujumbe usiku wa jana kutoka kwa XI JINPING wa China kwamba mkutano wake na KIM JONG UN ulikwenda vizuri sana na kwamba KIM anasubiri kwa hamu kukutana nami. China iliikabidhi Amerika Korea Kaskazini kama kafara kwa maslahi yake, ikiishinikiza Korea Kaskazini hadi kumfanya raisi wake kuwa tayari kulegeza msimamo na kukutana na majivuno Trump. Hususan kwa kuwa China tayari ishawahi kuhusika katika shinikizo la kisiasa, na katika kuchukua maamuzi katika Baraza la Usalama kuweka vikwazo kwa Korea Kaskazini. Hili limekuwa jambo muhimu katika kuifanya Korea Kaskazini kuwa tayari kulegeza msimamo juu ya mradi wake wa nuklia. Inaamini kuwa endapo itakosa uungwaji mkono na usaidizi wa China na China itafanya kazi kuidhibiti na kuizuia, hapo Korea Kaskazini itateseka! Hivyo basi Korea Kaskazini imelegeza msimamo! Wizara ya Kigeni ya China imefichua kuhusu dori yake ya ushawishi katika uamuzi wa Korea Kaskazini, ikitangaza hilo "Beijing imecheza dori murua juu ya bara la Korea" (Chanzo: Reuters, AFP, 23/5/ 2018). China imeonesha kuwa iko makini katika kupata maslahi yake ya kibiashara kwa Amerika zaidi ya washirika wake ambao haipati faida za kibiashara kutoka kwao, na huenda ikadhurika kibiashara kwa sababu ya hili, hata kama ni mwandani wa kikomunisti. Wasiwasi mkubwa wa dola ya kikomunisti umegeuka kuwa biashara na sio kulinda nchi nyenginezo za kikomunisti washirika wake! Kana kwamba China haitambui kuwa Amerika, huku ikitafuta kuinyang'anya silaha Korea Kaskazini, inatumia kadhia hii kuizunguka China na kuzuia udhibiti

*Endelea Uk..15*

wake wa bahari ya China Mashariki na Kusini!

4-Hili linathibitishwa na tangazo la China la kulikaribisha kongamano hili na kutangaza kuwa mshirika wake Korea Kaskazini imeachana na silaha zake za kinuklia kwa ajili ya Amerika. Balozi mkuu wa China na mshauri wa serikali, Wang Yi, alisema baada ya kongamano hilo: "Tunakaribisha na kuunga mkono matokeo yaliyo patikana katika kongamano hilo… Tunatarajia kuwa DPRK na Amerika zitafuatilia juu ya maafikiano ya pamoja yaliyoafikiwa na viongozi wao… katika kufikia kumaliza nuklia katika bara la Korea", aliongeza, "wakati huo huo, ipo haja ya kuweko mpangilio wa amani kwa bara la Korea kutuliza hofu ya kiusalama inayohisiwa na Korea Kaskazini." (Chanzo: Reuters, 12/6/201). Ikiwa China ilikuwa na utambuzi wa kutosha kisiasa na azma imara ya kisiasa, haingeishinikiza Korea Kaskazini, mshirika wake kwa njia hii! Lakini inathibitisha kuwa upeo wake na utambuzi wake wa kisiasa wa siasa za kimataifa bado ungali mwembamba na azma yake ya kisiasa ni dhaifu, kwa hivyo imefanya tu kwa kuchunga na kuhakikisha kuwa mahusiano yao ya kibiashara na Amerika ni mazuri kwa badali ya kuisalimisha Korea Kaskazini kwa Amerika, na wala haikuangalia mbele zaidi kwa lile ambalo hili litapelekea. Haitarajiwi kuwa Amerika inafanya kazi kuiteka Korea Kaskazini, kuileta karibu kwa ajili ya Amerika kuliko China, na kwamba Amerika inatafuta kupata umoja au muungano kati ya Korea mbili ili Korea mpya iwe nguvu ilio nje ya ushawishi wa China. Vietnam ni mfano usiokuwa wa mbali, ambayo ilikuwa hasimu kwa China baada ya Amerika kuziunganisha Vietnam Kusini na Kaskazini katika kongamano la Paris mnamo 1975!

5- China imecheza dori muhimu katika kuifanya Korea Kaskazini kukubali mkutano wa kongamano hilo kuiweka kadhia ya kuachana na silaha za kinuklia mezani pasi na kujadili pia Amerika kuachana na silaha za kinuklia. Amerika ni nchi pekee iliyozitumia na kueneza ufisadi ardhini, lakini shinikizo la China lilikuwa na athari ya kihakika! Kwa hivyo kongamano lilifanywa… Kongamano hilo lilitarajiwa kuchukua siku mbili lakini likafupishwa kuwa siku moja na muundo mpana ukakubaliwa, unaoashiria kasi ambayo Korea Kaskazini itaitikia yale Amerika inayoyataka. Korea kaskazini iliharibu kiwanda cha majaribio ya nuklia kuthibitisha azma yake ya kuachana na mradi wake wa nuklia, pamoja na kuwaacha huru Waamerika waliokuwa gerezeni mwake. Trump alieleza furaha yake kwa kile alichofaulu: "Ni mkutano murua sana. Maendeleo ni mengi mno". Huku Kim akilikadiria tukio hili la kihistoria alisema: "Ulimwengu utayaona mabadiliko makubwa". (Chanzo: Reuters, 12/6/2018). Wametia saini taarifa ya pamoja iliyo na nukta nne: Kwanza: pande mbili hizi zimejitolea kuasisi mahusiano mazuri kwa mujibu wa matarajio ya watu wao ya amani na ufanisi; pili: pande mbili hizi zitafanya kazi kuasisi na kuimarisha amani ya kudumu na utulivu kwa bara la Korea. Tatu: Korea Kaskazini ni lazima ijitolee kuchukua hatua za kuachana na silaha hizo kikamilifu katika bara la Korea. Nukta ya nne ilihusishwa na upande wa kibinadamu, kuahidi kurudisha mabaki ya Waamerika waliopotea na wafungwa tangu vita vya Korea na Amerika (1950-1953). Trump aliyasifu makubaliano hayo kuwa "mapana na muhimu mno" na Kim akaahidi katika taarifa "kuachana kikamilifu na silaha hizo katika bara la Korea". (Chanzo BBC, 12/6/2018). Taarifa hii yaashiria kuwa kuna muundo wa makubaliano, wala sio tu makubaliano juu ya nukta zinazofafanua yale yaliyoafikiwa juu yake, jinsi ya kutekeleza mpango wa kuachana na silaha hizo, mipangilio yake na muda na usimamizi wa utekelezwaji huo, na mambo mengine yanayohitajika na makubaliano hayo ambayo yaweza kutekelezwa mara moja kama ilivyokuwa katika makubaliano ya nuklia na Iran, ambayo maelezo yote haya yaliandikwa…

6- Hivyo basi, inatarajiwa kwamba Amerika itafanya majadiliano na mazungumzo marefu na Korea Kaskazini ambayo huenda yakachukua miaka mingi. Inaonekana kana kwamba Trump alitaka kukamilisha makubaliano ya mwanzo kwa haraka na kutatua tatizo hili na Korea Kaskazini, kwa kuwa tayari alikuwa ashafanya vitisho na hangeweza kurudi nyuma isipokuwa kufaulisha kitu kitakachoonesha amefaulu katika kuidhalilisha Korea Kaskazini. Kama tulivyo sema juu, lau si shinikizo la China, vitisho vya Trump havingepelekea kufanyika kwa kongamano hili na kutiwa saini kwa tangazo la Korea Kaskazini la azma yake ya kuachana na silaha za nuklia. Hivyo basi Trump ameweka rekodi ya ushindi wa kihistoria ambao huenda ukamfanya kufaulu katika raundi ya pili ya uchaguzi wa Uraisi wa Amerika utakapofanyika miaka miwili tu ijayo na kuziba sakata zote zilizojitokeza dhidi yake ambazo mpaka sasa bado hazijamalizika, na tuhuma za kufeli na kukashifiwa na wengine kwa kiburi chake na ubwege. Hili ni dhahiri kutokana na maneno ya Trump mwenyewe: "Usiniambie kuwa nchi yake tayari inaharibu kiwanda cha majaribio ya makombora … Tutaondoa vikwazo pindi tu tutakapopiga hatua muhimu katika kadhia ya kupunguza silaha za kinuklia… Bado hatujakata tamaa na chochote katika majadiliano haya… Tutakomesha mazoezi ya kijeshi tukiilenga Korea Kaskazini. Nitaitisha mkutano ikulului White House muda muwafaka utakapo wadia", pia alisema: "Alitia saini makubaliano ya kuachana na silaha za nuklia na UM kwa ajili ya kupunguza silaha hizo, nadhani tunao muundo wa kutayarisha upunguzaji silaha za nuklia kwa Korea Kaskazini". (Chanzo: Al-Jazeera, 12/6/2018). Hivyo basi Trump alitaka kumaliza faili ya mzozo na Korea Kaskazini, kuonesha kuwa amepata ushindi mkubwa.

7- Kumaliza faili ya mzozo na Korea Kaskazini au kuutuliza kunamsaidia Trump kujitolea katika vita vyake vya kibiashara na washirika wake na

*Endelea Uk..16*

maadui zake! Anamahusiano tata na washirika wake pindi alipotangaza kuwa ametoza ushuru mkubwa wa forodha katika biashara zao za madini ya Steel na Aluminium kutoka nje kuingia nchini mwake, ikizingatiwa kuwa makubaliano yao ya kibiashara yaliyotangulia yalikuwa na ubaguzi, aliandika katika mtandao wa Twitter mnamo 8/6/2018 alipokuwa akielekea katika kongamano la nchi kuu saba zenye uwezo mkubwa duniani (G7) jijini Quebec, Canada: "Akitarajia kuimarisha mikataba ya kibaguzi ya kibiashara na nchi hizo za G-7. Ikiwa hilo halitatokea, tutajitokeza vizuri zaidi!" Raisi wa Ufaransa Macron, na Waziri Mkuu Justin Trudeau, walizungumza katika mkutano wa pamoja wa waandishi habari wakikataa hatua hizi. "Hawako tayari kukubali kila kitu ili kutoa taarifa ya pamoja na Amerika", (Chanzo: AFP, 6/6/2018) Trump aliituhumu Ufaransa na Canada kutoza ushuru mkubwa kwa bidhaa za Amerika na kumtuhumu Waziri Mkuu wa Canada Trudeau kuwa "msumbufu".

"Kutakuweko na tofauti kubwa juu ya kadhia nyingi", afisa wa Canada aliwaambia maripota jioni ya Juni 7, 2018 (Chanzo: Reuters, 8/6/2018). Hata Raisi wa Ufaransa Macron, aliyefanya kazi juu ya maridhiano ya Kifaransa na Kiamerika, hakuweza kujimudu na kuendelea kutembea na Amerika na kuficha upinzani wake halisi, ambapo Ufaransa haikubobea kama Uingereza. Macron alisema: "Wanachama wengine sita wa G7 huenda wakaunda kundi lao wenyewe ikiwa kutakuwa na umuhimu", aliongeza kumkashifu Trump "Hakuna kiongozi anayedumu milele". (Chanzo: Reuters, 8/6/2018) Ujanja wa Uingereza ulijitokeza pindi Uingereza ilipotaka kuonesha kuwa haikubaliani na hisia hizi ili kudumisha mahusiano yake na Amerika huku ikichochea wengine dhidi yake. Waziri Mkuu May aliwaambia maripota: "Anataka Muungano wa Ulaya kujizuia kutokana na hisia zake dhidi ya ushuru wa Kiamerika na kwamba hisia hizi zapaswa kuwa za kisawa na halali" (Chanzo: Reuters, 8/6/2018). Chansela wa Ujerumani alisema katika mahojiano na runinga ya Ujerumani ya ARD mnamo 10/6/2018 juu ya uamuzi wa Trump wa kuondoa saini yake: "Kwa kweli, kuondoa huko, kupitia kuandika katika mtandao wa Twitter ni kwa kihakika na kwa kiasi fulani kuna vunja moyo, lakini huo sio mwisho". Waziri wa Kigeni wa Ujerumani Haiku Maas aliandika katika mtandao wa Twitter katika kujibu ufidhuli wa Trump, "kunaangamiza kiwango kikubwa sana cha imani". Uhasama huu unaolizunguka kongamano la G7 nchini Canada ulimazikia kwa kushambuliwa Trump na viongozi wa nchi nyenginezo zinazoshiriki kongamano hilo. Trump aliondoa saini yake katika taarifa ya pamoja ya kongamano la G7 na kumtuhumu Waziri Mkuu wa Canada aliyeongoza kongamano hilo kuwa "tapeli na dhaifu" (Chanzo: AFP, 10/6/2018). Trump aliwasili kwa kuchelewa katika kongamano hilo na kuondoka kabla ya kumalizika kwa kongamano hilo. Hivyo basi inaonekana kana kwamba vita vya kibiashara vimeanza, na vilitangazwa na Trump mnamo 2/3/2018 alipoandika katika mtandao wa Twitter: "Pindi nchi (Amerika) inapopoteza mabilioni ya dolari katika biashara na karibu kila nchi inayofanya nayo biashara, vita vya kibiashara ndio huwa bora, na rahisi kushinda". Yote haya yaonesha kuwa faili la vita hivi vya kibiashara ni muhimo mno kwa Amerika, huku ikiendelea kuteseka kutokana na matunda ya mgogoro wa kifedha uliolipuka mnamo 2008 huku madeni yakifikia zaidi ya dola trilioni 20, na Raisi Trump ambaye akili yake imetawaliwa na biashara anafanya kazi kuuokoa uchumi wa Amerika, akinyanyua mwito wa "Amerika kwanza". Hili linatishia kuvunjika kwa taasisi za kimataifa zilizotumiwa na Amerika tangu jadi kulazimisha ushawishi wake wa kiulimwengu na hivyo pasi kuvunjika kwa mfumo wa kiulimwengu na kuibuka kwa msimamo mpya wa kimataifa, ambapo Amerika haijitolei tena muhanga ili kubakia kuwa dola inayoongoza duniani, kwa usaidizi wa nchi nyenginezo na uvumilivu kupitia kuifanya mizani ya kibiashara kuwa upande wake, lakini inajali ubwana pekee pamoja na faida ya kibiashara pasi na usaidizi kutoka kwa washirika wake ili kuwaweka chini ya mwavuli wake na kutembea nyuma yake.

8- Amerika haijifungi na makubaliano yoyote na upesi hujiondoa au kuyatupilia mbali pindi inapo amini kuwa maslahi yake yanahitaji kujiondoa na kuvunja makubaliano hayo. Ilifanya hivyo kwa Korea Kaskazini mnamo 2003 chini ya George W. Bush, mwana, na kujiondoa kutoka katika makubaliano ya 1994 yaliyotiwa saini na Bill Clinton. Raisi wake wa sasa, Trump, alitia saini taarifa ya pamoja na washirika wake katika kongamano la G7 nchini Canada na kisha kuvunja makubaliano yake na kuondoa saini yake siku moja baadaye. Alivunja mkataba wa nuklia wa Iran uliotiwa saini na nchi yake chini ya Obama mnamo 2015. Makubaliano haya na Korea Kaskazini hayana dhamana na itatishia kuyavunja ili kuishinikiza Korea Kaskazini kuyatekeleza pindi majadiliano juu yake yanapoanza, kila inapopinga au kukataa kipengee chochote chake!

Uvunjaji mikataba na kiburi na kujiona tofauti na wengine na kuwatenza nguvu wengine yamekuwa ndio sifa ya kudumu ya Amerika, na yote haya ni nukta za kuporomoka, hivi karibuni… dola ya Khilafah Rashida itarudi kuwa ndio dola ya kwanza inayoongoza, kwa idhini ya Allah, kusimamisha uadilifu na kudumisha ahadi na kueneza uongofu na kutekeleza haki na kuondoa batili ikileta kheri kwa wanadamu na watu kuishi kwa usalama na amani katika nyanja zote. Mtume wa Allah (saw) ametoa bishara njema ya kurudi kwake baada ya utawala wa kiimla:

«ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ»"kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume", imesimuliwa na Ahmad kutoka kwa Hudhayfah (ra), na hili ni jepesi kwa Allah kulitimiza.

**2 Shawwal 1439 H**
**16/6/2018 M**



Email: info@uqab.or.ke